



REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

SECOND ASSEMBLY –FOURTH SESSION

THE HANSARD

Wednesday, 7th October 2020

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 3:30 p.m.*

[The Speaker (Hon. Kahindi) in the Chair]

PRAYERS

STATEMENTS

The Speaker (Hon. Kahindi): Is the Chairperson for Roads present? Anyone holding brief for him? Okay, also hon. Pascal is absent so we move his Statement next week. Next Order!

(Statements deferred)

MOTION

THE SECOND ADDRESS OF THE SECOND COUNTY ASSEMBLY BY THE GOVERNOR, KILIFI COUNTY
(WEDNESDAY AUGUST 26, 2020)

THAT, the Second Address of the Second County Assembly by His Excellency, Amason Jeffah Kingi, E.G.H, The Governor, Kilifi County (Wednesday August 26, 2020.)

THAT, Pursuant to the provisions of Standing Order No. 20 (5), the Thanks of the County Assembly be recorded for the exposition of public policy contained in the Second Address of the Second County Assembly by His Excellency, Amason Jeffah Kingi, E.G.H, The

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Governor, Kilifi County (Wednesday August 26, 2020) laid on the Table of this honourable House on Wednesday 30th September 2020.

(Hon. Ndago on 7.10.2020)

(Resumption of Debate interrupted on 7.10.2020)

Hon. Mramba: Asante sana Mheshimwa Spika, name naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Gavana na ni kwamba tumeweza kuona manufaa ya Ugatuzi na nilipokuwa kijana mdogo, niliwahi kuona gari ya kubeba wagonjwa ilikuwa moja tu kwa wilaya nzima. Leo hii tunavyoongea, magari ni mengi ila tutunapomsifu Gavana, pia tumjulishe kwamba kuna maafisa aambao wanafanya kazi kwa Kaunti hii ambao wanamvua mguu nyuma Gavana wetu jinsi anavyojaribu kwa uwezo wake, lakini kuna wachache ambao hawako tayari kuendeleza ile kazi yake. Hivyo basi, itakuwa ni lawama kwa sababu wananchi wanataka huduma na yeye ameweka mikakati mizuri lakini kuna watu wanamrudisha nyuma.

Nikipeana mfano kwa kitengo cha Afya, tumeona kwamba juzi motto mmoja aliumwa na nyoka kule Kathama hiyo iko Wadi ya Adu. Kijana Yule aliaga dunia kwa sababu mhudumu wa hospitali alipiga simu apate gari ya kubeba mgonjwa lakini gari ambayo iko Baolala ni mbovu. Ni kifaa kidogo cha shilingi elfu thelathini (30,000) ambacho kimeharibika lakini hakijatengenezwa hatimaye walipopata gari nyingine kufika mjiwa Malindi, motto ameaga. Sasa ni mambo madogo ambayo yanaleta ulegevu na sifa mbaya kwa Kaunti yetu ya Kilifi.

Tukienda kwa upande wa Kilimo, Mheshimiwa Gavana amenena kwamba amejaribu kupena chakula kwa maeneo kame lakini pia tukubali pia hilo sio suluhisho. Suluhisho ni kuona kwamba yale maeneo yanaweza kuwezesha na wakulima wakazalisha chakula. Huwezi kunipatia mfano kama Wadi za Sabaki ama Jilore ama Garashi kwamba watu kama wale wapelekewe chakula cha msaada. Si haki kwa sababu udongo uko na rotuba, wao ni wakulima kwa bidii. Wale ni watu wa kuwezesha kupatiwa jembe waweze kuzalisha chakula kinachoweza kulisha watu wengine ambako labda sehemu kama Bamba ambako mvua yao haitabiriki, tunaweza kuwalisha sisi watu wa Kakuyuni ikiwa tutawezeshwa. Lakini tununue magunia ya mahindi, maharagwe kupelekea watu wa Madunguni na wao wenyewe wako na ardhi ambayo iko na rotuba nyingi sana. Sehemu ya Chakama ambayo iko Wadi ya Adu wako na watu ambao wakiwezeshwawa tutengeneza chakula kingi sana.

Lakini utaona lile tinga linakuja pale nikipeana mfano kwa Wadi yangu, tinga lilikuja siku moja likalima shamba langu mimi na ni miujiza kwa sababu lililima ekari tatu kwa siku nzima na likimaliza kulima tinga linaondoka likiwa limeharibika mpaka awamu ilipoisha. Sasa sisi tunawawekea pesa za kununua matinga ili wananchi waweze kulimiwa kwa bei nafuu. Lakini ukiangalia ile *management* ya zile *tractors*, mimi maoni yangu naona ule mradi wa matinga uondolewe wanachi wajue hakuna tinga za kaunti kuliko ziwe pale na hakuna faida yoyote. Mkulima yoyote ambaye atategemea tinga la kaunti, haki ya Mungu atafaili kabisa kwa sababu tinga linaweza kuja siku moja na Yule dereva anaingia saa mbili kwa sababu yeye amejiri wana Kaunti ikifika saa kumi amefunga kazi mpaka kesho. Lile tinga lililima shamba moja ekari kama nne ama tano bila kuharibika, basi ni miujiza sana.

Bw. Spika, mimi ninamaoni kwamba Bw. Gavana anafanya kazi nzuri lakini ni lazima Kamati zetu za Bunge zifanye kazi ya *oversight* kwa Mawaziri na *Chief Officers* wa Idara.

Disclaimer: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.

La mwisho, tunakubali kwamba Gavana wetu amefanya mabadiliko kipindi cha kwanza alisisitiza zaidi Mtwapa, Kilifi, Malindi. Barabara ziko sawa siwezi sema ziko asilimia kwa mia, lakini nasisi ambao tunatoka zile wadi za mashinani, tunahitaji watu wetu wakanyage lami. Lami haiwezi kuwa imetengezwa kwa watu wa tauni, watu wa Kakuyuni, Madunguni, Kavunyalalo, Mangani wana haki ya kukanyaga lami kwa sababu ni wapiga kura na wanalipa ushuru sawa sawa na watu wa Shella na Shimo la Tewa. Kwa hivyo, ikiwa tulikupatia nafasi umetengeza ile miji, lakini nasisi safari hii tuangalie kule mashambani angalau tupate barabara nzuri.

Ikiwa mavuno yametoka Madunguni ni tomato alafu zikose barabara, zitafikaje Kongowea? Sasa tomato zitaharibikia barabarani kwa sababu hakuna barabara. Ninachoomba Waheshimiwa safari hii Bw. Amason Jeffah amefanya kazi nzuri na anaenda kupumzika, tutafute Gavana amabaye atakuwa na maono kama ya Kingi ili aanzie pale alipoishia Kingi aweze kutupeleka mbele. Kuna wengine wanataka Ugavana lakini wanapopata Ugavana, wataturudisha hatua tatu nyuma. Naomba tuwe na hekima ya kuchagua Gavana atakayetuchukua pale alipoishia Gavana Kingi tuende mbele ili kazi yetu iweze kuwa nzuri.

La mwisho, namuomba Mheshimiwa Stanley Karisa Kenga ambaye ni Mjumbe wa Adu nimeambiwa na yeye mwenyewe pia aliniambia nimesikia vikao vyake anataka kwenda Bunge kule Nairobi na Mheshimiwa Matsaki na Pascal Thuva, mwendapo kule mkumbuke kutetea ugatuzi ueze kuendelea. Asante sana.

(Hon. Kenga stood on a Point of Order)

Hon. Kenga: Mheshimiwa Spika, niseme kwamba hata kama tunaenda Bunge la Kitaifa, Seneti ndio wanatetea Kaunti.

(Laughter)

The Speaker (Hon. Kahindi): Yes Hon. Benson (Chengo).

Hon. Chengo: Asante Mheshimiwa Spika. Pia mimi nimesimama kuunga mkono hii hotuba ya Gavana wetu ya kwamba kuna vitu vimeonekana vimefanyika ambavyo wananchi wetu wa Kilifi wanafurahia. Mimi langu ni kwamaba ile barua ambayo inasema miradi mengine isifanyike inatumiza sana. Naamini kwamaba Gavana akituruhusu kwendela kujenga hizo hospitali zinaweza kutusaidia sana. Kumalizia ni kwamaba nataka nimshukuru Gavana wetu kwa kazi nzuri.

Hon. Mwambire: Asante Mheshimiwa Spika kwa nafasi hii. Kwanza ningependa kuchukua nafasi hii kupongeza hotuba ambayo imegusia utenda kazi wetu na ushirikiano. Pia ningependa kumshukuru Gavana kwa kuangalia Wadi yangu upande wa afya kuna sehemu ambayo ilikua wanatembea masaa saba, Shirango *Dispensary* ambayo ilifadhiliwana *Kenya Marine Fisheries* na *County Government* iliweza kufunguliwa mwaka jana.

Pia upande wa mabarabara nashukuru Gavana ameweza kuongea na Rais wetu wa Kenya kwamba sehemu ya barabara kutoka Bamba mpaka Lango Baya itawekwa lami na nataka kumshukuru Rais wetu aliweza kukiri kwamba ataitengeneza na pia barabara ya kutoka Bamba kwenda Ganze.

Ningependa pia, kumshukuru Gavana kwa upande wa *youth polytechnic*, kuna *youth polytechnic* kumi na nne (14) ziliweza kufaidika na vifaa vya ufundi kwa vijana wetu.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Ningependa kuomba kupitia Idara ya *Education and ICT* waweze kuangalia mbinu ya kuchukua vijana kwa *youth polytechnic* ambao waliomaliza kidato cha mne mekanika wengi katika county hii, ili waweze kupata kujifundisha ufundi katika *youth polytechnic* zetu. Asante Mheshimiwa Spika

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

POSTPONEMENT OF THE COMMITTEE OF THE WHOLE HOUSE ON THE KILIFI COUNTY CITIZEN PARTICIPATION AND CIVIC EDUCATION BILL 2019

The Speaker (Hon. Kahindi): Honourable Members, there was a Committee of the Whole House, but I noticed that the Report has just been Tabled; I want to give Members at least one week for them to go through the Report before we can proceed with it.

ADJOURNMENT

In the absence of any other business in the Order Paper, the House Stands adjourned. The official communication will come from the Clerk on tomorrow's engagement. Thank you very much.

The House rose at 4.06 p.m.

Disclaimer: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.